رئاسة الشؤون الدينية
بالمسجد الحرام والمسجد النبوي

فَضَائِلُ وَآدَابُ المَسْجِدِ النَّبَوِيِّ وَأَحْكَامُ زِيَارَةِ قَبْرِ النَّبِيِّ ﷺ وَقَبْرَي صَاحِبَيْهِ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمَا

سواحلي

Kiswahili

Fadhila na adabu za Msikiti wa bwana Mtume na hukumu za kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na kaburi za Maswahaba zake wawili, Mwenyezi Mungu awe radhi nao

Kamati ya Kielimu ya Uongozi wa Masuala ya Kidini katika Msikiti Mtukufu wa Makka na Msikiti wa Mtume

فَضَائِلُ وَآدَابُ المَسْجِدِ النَّبَوِيِّ
وَأَحْكَامُ زِيَارَةِ قَبْرِ النَّبِيِّ ﷺ
وَقَبْرَي صَاحِبَيْهِ رَضِيَ اللهُ عَنْهُمَا

Fadhila na adabu za Msikiti wa bwana Mtume na hukumu za kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na kaburi za Maswahaba zake wawili, Mwenyezi Mungu awe radhi nao

اللَّجْنَةُ العِلْمِيَّةُ

بِرِئَاسَةِ الشُّؤُونِ الدِّينِيَّةِ بِالمَسْجِدِ الحَرَامِ وَالمَسْجِدِ النَّبَوِيِّ

Kamati ya Kielimu ya Uongozi wa Masuala ya Kidini katika Msikiti Mtukufu wa Makka na Msikiti wa Mtume

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Fadhila na adabu za Msikiti wa bwana Mtume na hukumu za kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na kaburi za Maswahaba zake wawili, Mwenyezi Mungu awe radhi nao

Utangulizi

Kila sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu, na rehema na amani zimfikie yule aliyetumwa kuwa rehema kwa walimwengu wote, na kwa familia yake, na Maswahaba wake, na wale waliofuata mwenendo wake, na wakaongoka kwa muongozo wake, mpaka Siku ya Malipo. Ama baada ya hayo:

Huu ni ujumbe mfupi, uliokusanya fadhila muhimu za Msikiti wa bwana Mtume, na adabu za kuutembelea, na adabu za kulitembelea kaburi la bwana Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na makaburi ya maswahaba wake wawili. Tumezikusanya kwa ajili ya wenye kuutembelea Msikiti wa bwana Mtume; ili wawe na elimu na utambuzi wa fadhila za msikiti wa Mtume wa Umma huu, rehema na amani za Mwenyezi Mungu

ziwe juu yake, na adabu za kuutembelea na kuswali ndani yake, tukitarajia kutoka kwa Mkarimu, Mwingi wa kuneemesha awanufaishe kwa ujumbe huu, na aufanye kuwa wenye kufaa, na uwe kwa ajili ya kutaka radhi zake tu. Kwani, Yeye ndiye mbora wa wenye kuombwa, na Mkarimu zaidi mwenye kutarajiwa.

Kamati ya elimu

Ya kwanza: Fadhila za Msikiti wa Mtume

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿وَرَبُّكَ يَخۡلُقُ مَا يَشَآءُ وَيَخۡتَارُۗ مَا كَانَ لَهُمُ ٱلۡخِيَرَةُۚ سُبۡحَٰنَ ٱللَّهِ وَتَعَٰلَىٰ عَمَّا يُشۡرِكُونَ ٦٨﴾

Na Mola wako Mlezi huumba na huteuwa atakavyo. Viumbe hawana khiari. Mwenyezi Mungu ametukuka na ametakasika na hao wanao washirikisha naye. [Al-Qasas: 68] Na Mwenyezi Mungu amepachagua mahali hapa kuwa msikiti wa Nabii wake – Rehema na Amani zimshukie – na amepahusisha kwa fadhila nyingi, miongoni mwazo ni:

Kwamba ni miongoni mwa misikiti mitatu inayofungiwa safari:

Imepokewa kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake-: “Hazifungwi safari

isipokuwa kwenda kwenye Misikiti mitatu: Msikiti wangu huu, Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Al-Aqsa.”[1]

Ya kwamba kuswali ndani yake ni bora kuliko swala elfu moja katika misikiti mingine isipokuwa Msikiti wa Makka:

Na kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- hakika Mtume -Rehema na amani za Allah ziwe juu yake- Amesema: "Kusali ndani ya Msikiti wangu huu ni bora kuliko sala elfu moja zinazoswaliwa nje ya Msikiti huu isipokuwa Msikiti wa Makka."[2]

Kwamba ni Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa uchamungu tangu siku ya mwanzo:

Kutoka kwa Abuu Saidi Al Khudriy Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: Amesema: Niliingia kwa Mtume Rehema na Amani zimshukie katika nyumba ya mmoja wa wakeze, nikasema: Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, ni upi kati ya misikiti miwili ambao uliasisiwa juu ya uchamungu? Akasema: Basi akachukua choto la changarawe, akapiga nalo ardhini, kisha akasema: “Ni Msikiti wenu huu,” yaani Msikiti wa Madina[3].

---

[1] Ameitoa Bukhari,kwa nambari (1189), na Muslim, nambari (1397) na Tamko ni la Muslim.

[2] Imepokelewa na Bukhari, kwa nambari (1190), na Muslim, nambari (1395), na tamko ni la Bukhari.

[3] Imepokelewa na Muslim,kwa nambari (1398).

Nikuwa malipo ya mwenye kutafuta elimu ndani yake, ni kama malipo ya mpiganaji katika njia ya Mwenyezi Mungu:

Imepokewa kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Nilimsikia Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- akisema: "Yeyote mwenye kuja katika Msikiti wangu huu, hakuja isipokuwa kwa ajili ya kheri anayojifunza au kuifundisha, basi huyo yuko katika daraja la mpiganaji Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu, na mwenye kuja kwa ajili ya jambo lisilokuwa hilo, basi yeye yuko katika daraja la mtu anayeangalia mali ya mwenzake"[1].

Kwamba ndani yake ipo Raudhwa tukufu:

Na imesimuliwa kutoka kwa Abuu Huraira, Mwenyezi Mungu amridhie, kutoka kwa Mtume rehema na amani ziwe juu yake amesema: “Nafasi iliyoko baina ya nyumba yangu na mimbari yangu ni bustani miongoni mwa bustani za Peponi, na mimbari yangu iko juu ya Hawdhi yangu.”[2]

[1] Imepokelewa na Ibn Majah,kwa nambari (227), kwa sanadi sahihi.
[2] Wamekubaliana Hadithi hii Bukhari kwa nambari 1195 na Muslim kwa nambari 1390.

Pili: Inapendekezwa kuutembelea Msikiti mtukufu wa Mtume

Kwa fadhila hizi na nyinginezo, inapendekezwa kuutembelea Msikiti wa Mtume ili kuswali humo na kufanya ibada.

- Ni Sunna kwa mwenye kuhiji na asiyekuwa yeye kuzuru Msikiti wa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kabla ya Hija au baada yake, na ziara hii si katika masharti ya Hija wala nguzo zake wala wajibu zake, na wala haina mafungamano nayo.

- Wala haishurutishwi katika kuutembelea Msikiti wa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- idadi maalum ya Swala, au kukaa muda maalum Madina,isipokuwa ziara inatimia kwa kuswali swala moja, sawa iwe ya faradhi au ya hiari, lakini kadiri Swala zinavyozidi humo, ndivyo malipo yanavyoongezeka.

- Inapendekezwa kwa mwenye kuzuru Msikiti wa Mtume kuswali humo Swala zote za faradhi na vile vile swala za sunna; kwani Swala ndani yake ni bora kuliko swala elfu moja katika misikiti mingineyo isipokuwa Msikiti Mtukufu wa Makka.

Tatu: adabu za kuutembelea Msikiti wa Mtume

Anapofika Muislamu katika Msikiti wa bwana

Mtume, inapendeza kwake ajipambe na adabu za kisheria zinazofungamana na Misikiti kwa ujumla, na hasa Msikiti wa bwana Mtume, nazo ni:

Aende Msikitini kwa utulivu, na heshima, na twahara, na muonekano mzuri, na harufu nzuri, na imepokewa kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: «Itakapokimiwa swala, basi msiijie swala hiyo huku mnakimbia, na iendeeni mkiwa na utulivu, basi kile mtakachokiwahi swalini, na kile kitakachowapita timizeni, kwani hakika mmoja wenu anapoikusudia swala, huwa yuko katika swala»[1]، Na imesimuliwa kutoka kwa Abuu Sa'id Al-Khudri, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kwamba Mtume rehema na amani ziwe juu yake, alisema: "Josho la siku ya Ijumaa ni wajibu kwa kila aliyejiotea, na apige mswaki, na apake marashi akiyapata"[2],"" Ama mwanamke anapokuja Msikitini, inapaswa kwake kujisitiri kwa hijabu yake, na haifai kwake kujitia manukato; kwa sababu ya kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake: ""Atakapohudhuria mmoja

[1] Imepokelewa na Bukhari, kwa nambari (636), na Muslim, kwa nambari (602).

[2] Wamekubaliana juu ya Hadithi hii, Bukhari kwa nambari 846, na Muslim kwa nambari 858, na Muhtalim ni aliyebaleghe.

wenu msikitini, basi asiguse manukato."[1]"

Inapendekezwa kwa mwenye kuzuru kwamba autangulize mguu wake wa kulia anapoingia Msikiti wa Mtume, kama ilivyo katika misikiti mingine, na aombe dua hii: «Bismillah, was-salaamu 'alaa Rasuulillah, Allahumma-ghfir liy dhunuubiy waftah liy abwaaba rahmatika» Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na salamu zimshukie Mtume wa Allah, Ewe Mola nisamehe madhambi yangu na unifungulie milango ya rehema zako (9).[2] Na vile vile atasema: "Ninajilinda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa uso wake Mkarimu, na kwa ufalme wake wa enzi, kutokana na shetani aliye laaniwa."[3]

Kuswali salamu ya msikiti: Ni sunna kwa mwenye kuingia Msikiti wa Mtume kwa ajili ya kuswali humo, aswali rakaa mbili za salamu ya msikiti kabla ya kukaa, imepokewa kutoka kwa Abu Qatada Al-Haarith bin Rib'iy Al-Answaariy -Radhi za Allah ziwe juu yake-, amesema: Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: ""Atakapoingia mmoja wenu msikitini, basi

[1] Imepokelewa na Muslim,kwa nambari (443).
[2] Imepokelewa na Ibn Majah, nambari (771), kwa sanad sahihi.
[3] Imepokelewa na Abu Daawuud, nambari (466), kwa msururu sahihi wa upokezaji (sanad).

asikae mpaka aswali rakaa mbili."[1]"

Himizo la kuswali katika swafu za kwanza; kwakuwa ndani yake kuna fadhila kubwa, na jambo hilo haliwi isipokuwa kwa kuwahi, kwa hadithi ya Abu Huraira radhi za Allah ziwe juu yake: kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu, rehema na amani ziwe juu yake amesema: "Lau watu wangelijua fadhila zinazo patikana katika Adhana na safu ya kwanza, kisha wakawa hawana budi ila kupiga kura juu yake, basi wangepiga kura."[2], Na kwa kauli ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kwa Maswahaba wake, Mwenyezi Mungu awe radhi nao: “Songeni mbele na mnifuate, na wakufuateni nyinyi wale walio baada yenu. Na watu wataendelea kuchelewa mpaka Mwenyezi Mungu awacheleweshe.”[3]

Ama wanawake basi lililo bora kwao ni kuswali katika safu za nyuma, na kuwa mbali na wanaume, kwa hadithi ya Abuu Huraira Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, Amesema: Amesema Mtume wa mwenyezi mungu rehema na amani ziwe juu yake: ""Safu bora kwa wanaume ni safu ya kwanza, na safu

[1] Wamekubaliana juu ya Hadithi hii Bukhari kwa nambari 1171, na Muslim kwa nambari 714.

[2] Wamekubaliana juu ya usahihi wa Hadithi hii, Bukhari kwa nambari 615, na Muslim kwa nambari 437.

[3] Imepokelewa na Muslim, kwa nambari (438).

yenye shari ni ya nyuma, na safu bora kwa wanawake ni safu ya mwisho na yenye shari ni safu ya mwanzo""[1]، Lakini ikiwa wataswali wakiwa wametengana, au baina yao na wanaume kuna kizuizi, kama ilivyo katika Msikiti wa Mtume, basi safu bora kwao ni ya kwanza; kwa kuondoka kwa sababu ya hilo.

Kuswali nyuma ya imamu, na kujihadhari na kumtangulia; kwa hadithi ya Abu Huraira Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake kwamba Mtume - Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: "Hakika amefanywa imamu kuwa ni mwenye kufuatwa."[2].

Wala haifai kwa mwenye kuswali kumtangulia Imamu isipokuwa katika hali ya dharura na msikiti kujaa wenye kuswali, kiasi kwamba hapati mahala pa kuswalia isipokuwa mbele ya Imamu.

Kujitahidi kuziba mapengo baina ya safu na kuzinyoosha, lakini kwa tahadhari ya kutowasonga watu na kuwadhikisha, na kuruka shingo zao, na kupita mbele ya wenye kuswali; kwa kuwa kufanya hivyo kunamtia mtu katika dhambi.

Kuswali katika Raudhwa tukufu kwa yule aliyewezeshwa hilo; kwa sababu ya hadithi ya Abu

[1] Imepokelewa na Muslim,kwa nambari (440).
[2] Imepokelewa na Bukhari, nambari (722), na Muslim,kwa nambari (417).

Hurairah, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kwamba Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, amesema: “Nafasi iliyoko baina ya nyumba yangu na mimbari yangu ni bustani miongoni mwa bustani za Peponi, na mimbari yangu iko juu ya Birika langu.”[1]

Haijapokelewa fadhila maalumu kuhusu kuswali katika Raudhwa, lakini imethibiti kuwa ni bustani miongoni mwa mabustani ya Peponi -kama inavyojulisha Hadithi ya Abu Huraira, Mwenyezi Mungu awe radhi naye, iliyotangulia- na ibada hupata fadhila kutokana na fadhila ya wakati wake na mahali pake.8

Na mgeni achague nyakati maalumu za kuswali katika Raudhwa, na apupie nyakati ambazo msongamano unapungua, kwani haifai kuwasongamanisha ndugu zake waislamu, wala asiwaruke watu, wala asipite mbele ya wanao swali kwa ajili ya kuswali humo. Kuswali katika Raudhwa ni swala ya Sunna, hivyo jambo hilo la sunna halifikiwi kwa kufanya jambo la haramu. Vilevile, mgeni ajitahidi kufuata na kuzingatia nidhamu maalum na taratibu zilizopangwa kwa ajili ya kuingia katika Raudhwa, na kuchagua nyakati maalumu, na kutoa ushirikiano kwa

[1] Wamekubaliana juu ya Hadithi hii, Bukhari kwa nambari 1195, na Muslim kwa nambari 1390.

wanaosimamia mpangilio wa kuingia wageni humo.

Kufaidika na nyakati kwa kukithirisha matendo mema yanayomkurubisha kwa Muumba wake Subhanahu, kama vile swala, kusoma Qur'ani, dhikri, dua, kuhudhuria majilisi za dhikri, durusi za elimu, halaka za kufundisha Qur'ani Tukufu, na mengineyo.

Kuheshimu Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu na kukihifadhi kutokana na kuchezewa kwa kurasa zake, kukiandikia, au kukidhalilisha na kukivunjia heshima kwa kuweka viatu pembezoni mwake, au kukiweka ardhini na mfano wa hayo, kwa kauli Yake Mtukufu:

﴿ذَٰلِكَ ۖ وَمَن يُعَظِّمْ شَعَـٰٓئِرَ ٱللَّهِ فَإِنَّهَا مِن تَقْوَى ٱلْقُلُوبِ﴿٣٢﴾﴾

Ndio hivyo! Na anayetukuza ibada za Mwenyezi Mungu, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo.

[Surat Al-Hajj: 32].

Kuinamisha macho kutokana na yale aliyoyaharamisha Mwenyezi Mungu Mtukufu: Inamlazimu mtembeleaji wa Msikiti wa Mtume kuinamisha macho yake kutokana na yale ambayo si halali kwake kuyatazama. Na anapaswa kujua ukubwa wa kutenda dhambi katika maeneo haya matakatifu, na adhabu zinazoambatana nalo. Kwani madhambi huwa makubwa zaidi kutokana na utukufu wa wakati na mahali, na vivyo hivyo matendo ya utiifu. Na

mwanamke Muislamu ajitahidi kushikamana na Hijabu ya kisheria, na kutodhihirisha mapambo ili asiwajaribu wanaume, kwani jambo hili dhambi yake ni kubwa.

Tahadhari ya kujishughulisha na kupiga picha au kutazama picha na video katika simu, na jambo hilo linakuwa zito zaidi pindi picha na video hizi zinapokuwa zimeharamishwa.

Kuutakasa Msikiti wa Mtume kutokana na kila lisilofaa miongoni mwa ugomvi, na kunyanyua sauti, na kutangaza kilichopotea, na kuuza, na mfano wa mambo hayo ambayo hayapasi ndani yake wala katika misikiti mingine; kwa hadithi ya Abu Huraira, Mwenyezi Mungu awe radhi naye, kutoka kwa Mtume ﷺ kwamba amesema: "Mtakapomwona anayeuza au kununua msikitini, basi semeni: Mwenyezi Mungu asiitie faida biashara yako, na mtakapomwona anayekitangaza kilichopotea humo, basi semeni: Mwenyezi Mungu asikurudishie."[1]

Kutilia maanani usafi wa mwili, na kujihadhari na harufu mbaya kama vile kitunguu saumu na kitunguu maji, moshi na jasho, na mfano wa hayo katika yale yanayosababisha udhia kwa ndugu zake wenye

[1] Imepokelewa na At-Tirmidhiy, nambari (1321), na Ibn Khuzaymah, nambari (1305), kwa sanadi sahihi.

kuswali; kwa hadithi ya Jabiri bin Abdillah -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- alisema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu -Rehema na Amani ziwe juu yake- alisema: «Atakayekula kitunguu saumu, au kitunguu maji, basi na ajitenge nasi, au ajitenge na msikiti wetu, na akae nyumbani kwake»[1].

Kuhakikisha usafi wa Msikiti wa Mtume na kutotupa takataka ndani ya Msikiti na katika maeneo yake, kama vile mabaki ya vyakula na mikeka ya futari, hasahasa katika mwezi wa Ramadhani, au kutema mate katika njia na maeneo yake, na mfano wa hayo.

Epuka kuswali katika sehemu za kupita watu, na mlangoni, na sehemu zenye msongamano, ili kuepuka kuleta madhara, na kuziba njia, na kuwaudhi Waislamu.

Swala ya wanaume na wanawake iwe katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kila mmoja wao, ndani ya Msikiti wa Mtume au katika viwanja vyake, na mwanamume asiswali pembeni mwa mwanamke, wala mwanamke pembeni mwa mwanamume, na tahadhari dhidi ya kumtangulia Imamu iwezekanavyo.

Kutanguliza mguu wa kushoto wakati wa kutoka Msikitini, na atasema: "Ewe Mwenyezi Mungu hakika

[1] Imepokelewa na Bukhari,kwa nambari (7359), na Muslim,kwa nambari (564).

mimi ninakuomba unipe katika fadhila zako"[1], Au atamswalia Mtume - rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - kwa kusema: "Ewe Mola wangu nisamehe madhambi yangu, na unifungulie milango ya fadhila zako".[2]

Ya nne: Hukumu na adabu za kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na makaburi mawili ya Maswahaba zake wawili, Mwenyezi Mungu awe radhi nao.

Inapendeza kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na makaburi ya Maswahaba wake wawili: Abubakari na Omari, Mwenyezi Mungu awe radhi nao, kwa ajili ya wakazi wa Madina na kwa yule anayeifika akiwa mgeni na mtembeleaji; kwa mujibu wa dalili za jumla zinazojulisha uhalali wa kuzuru makaburi, na miongoni mwazo ni kauli yake, rehema na amani ziwe juu yake: «Nilikuwa nimekukatazeni kutembelea makaburi. Basi yatembeleeni»[3].

Na kinachojulisha fadhila za kumtakia Salaam Mtume rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe

[1] Imepokelewa na Muslim, nambari (713).
[2] Imepokelewa na At-Tirmidhiy, nambari (314), kwa sanadi sahihi.
[3] Imepokelewa na Muslim, kwa nambari (977).

juu yake baada ya kifo chake, ni kauli yake -Rehema na amani ziwe juu yake-: ""Hakuna yeyote atakayenisalimia isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hunirudishia roho yangu ili nimjibu salamu."[1]"

Na haifai kisheria kwa wanawake kuzuru kaburi lake, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, wala kaburi la Muislamu mwingine yeyote. Kwa hakika, kuzuru makaburi kumewekewa wanaume. Ama wanawake, wao walikatazwa kuzuru makaburi; kutoka kwa Ibn Abbas, Mwenyezi Mungu awawie radhi wote wawili, amesema: "Amewalaani Mtume -Sala na Amani ziwe juu yake- (wanawake) wenye kuzuru makaburi, na wenye kuyafanya kuwa mahala pa ibada (misikiti) na kuweka juu yake taa"[2] Na imepokewa kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake-: "Amewalaani Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- wanawake wenye kuzuru makaburi"[3].

Na hairuhusiwi kufunga safari kwa ajili ya kulizuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi

---

[1] Ameipokea Ahmad, katika Al-Musnad kwa nambari: (10815), kwa Isnad Hasan.

[2] Imepokelewa na Abu Daawuud,kwa nambari (3236), na At-Tirmidhiy,kwa nambari (320), na An-Nasaai,kwa nambari (2043).

[3] Imepokelewa na At-Tirmidhiy, nambari (1056), na Ibn Maajah, nambari (1576), kwa isnaad hasan.

Mungu ziwe juu yake, kwa kunuia katika safari yake kulizuru kaburi peke yake. Bali ananuia kwa safari yake kuutembelea Msikiti na kuswali ndani yake. Basi anapokuwa ametulia Madina, anaruhusiwa kisheria kulizuru kaburi, kama inavyoruhusiwa kisheria kwa wakaazi wa Madina miongoni mwa watu wake; Kama alivyosema Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake: "Hazifungwi safari isipokuwa kwenda kwenye Misikiti mitatu: Msikiti wangu huu, Msikiti Mtakatifu na Msikiti wa Al-Aqsa."[1]

Adabu za kisheria wakati wa kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na makaburi mawili ya Maswahaba zake wawili, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao.

Mfanya ziara atasimama mbele ya kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, huku akilielekea kaburi, kisha atamsalimia Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kwa heshima na kushusha sauti, akisema: (Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, na rehema zake na baraka zake). Na ikiwa atazidisha juu ya hilo na kusema: (Ninashuhudia kwamba hakika ulifikisha Ujumbe, na ukatekeleza Amana, na ukaunasihi Umma, na ukapigana jihadi kwa

[1] Imepokelewa na Bukhari, nambari (1189), na Muslim, nambari (1397) na Tamko ni la Muslim.

ajili ya Mwenyezi Mungu haki ya kupigana) basi hakuna ubaya katika hilo; kwa sababu haya yote ni haki.

Kisha atapiga hatua moja kuliani kwake ili aweze kulielekea kaburi la Abubakari Swiddiq, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Atasema: "Assalaamu 'alaika yaa Abaa Bakri Swiddiiq, Assalaamu 'alaika yaa Khaliifata Rasuulillaah swalla llaahu 'alaihi wasallam, radhwiyallaahu anka wa ardhwaaka, wajazaaka an Ummati Muhammadin swalla llaahu 'alaihi wasallam khairaan." Yaani: "Amani iwe juu yako ewe Abubakari Swiddiq, Amani iwe juu yako ewe Halifa wa Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, Mwenyezi Mungu akuridhie na akuridhishe, na akulipe kwa niaba ya Umma wa Muhammadi, rehema na amani ziwe juu yake, kheri nyingi."

Kisha atapiga hatua moja kuliani kwake ili alielekee kaburi la Omari bin Al-Khattwab, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na atasema: "Assalaamu 'alaika yaa 'Umaral Faaruuq, radhwiyallaahu 'anka wa ardhwaak, wajazaaka 'an ummati Muhammadin swallallaahu 'alayhi wasallam khairaa." Yaani: "Amani iwe juu yako ewe Omar Al-Faruuq, Mwenyezi Mungu akuridhie na akuridhishe, na akulipe kwa niaba ya Umma wa Muhammadi, rehema na amani ziwe juu

yake, kheri nyingi."

Na bin Omari, Mwenyezi Mungu awe radhi nao wote wawili, aliporudi kutoka safarini, alikuwa akifika kwenye kaburi la Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, na akasema: "Amani iwe juu yako, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Amani iwe juu yako, ewe Abubakari. Amani iwe juu yako, ewe baba yangu. Kisha anaondoka"[1].

Haifai kugusa kuta za kaburi wala uzio, wala kuvibusu:

Amesema Imam Malik, Mwenyezi Mungu amrehemu: "Anapomsalimu Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- atasimama na uso wake uelekee kaburini; na siyo kuelekea Qibla, atasogea karibu na kutoa salamu na wala asiguse kaburi kwa mkono wake"[2].

Na Maimamu wamekubaliana kwamba haifai kuligusa kaburi la Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kwa mkono wala kulibusu.

Hakai muda mrefu kaburini, bali anatoa salamu kisha anaondoka.

Amesema imamu Maalik, Mwenyezi Mungu

[1] Imepokelewa na Al-Baihaqī katika As-Sunan Al-Kubra, nambari (10271), kwa sanad sahihi.

[2] Tazama: Ash-Shifaa cha Al-Qaadhi 'Iyaadh, uk. (2/ 199).

amrehemu: “Sioni kuwa asimame kwenye kaburi la Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, akiomba dua, lakini atoe salamu na aondoke”[1].

Na amesema Naafi Allah amrehemu: "Alikuwa bin Omari akitoa salamu kaburini.. nimemuona mara mia moja na zaidi akija kwenye kaburi na kusema: Amani iwe juu ya Mtume, rehema na amani ziwe juu yake. Amani iwe juu ya Abu Bakar, Amani iwe juu ya baba yangu, kisha anaondoka"[2].

Ama yale wanayofanya baadhi ya wenye kuzuru ya kuinua sauti zao kwenye kaburi lake, rehema na amani ziwe juu yake, na kusimama hapo kwa muda mrefu, hili ni kinyume na ilivyoamrishwa.

Hairuhusiwi kumuomba Mtume rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake wala kiumbe mwingine yeyote alete manufaa au aondoe madhara, au atimize haja, au aondoe dhiki, au amponye mgonjwa, au aombee uombezi, au aokoe na adhabu, au mfano wa hayo. Kwa sababu kumuomba asiyekuwa Mwenyezi Mungu katika yale ambayo hakuna mwenye uwezo nayo isipokuwa Mwenyezi Mungu ni haramu na shirki kubwa, amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

---

[1] Tazama: Ash-Shifaa cha Qaadhi 'Iyaadh, uk. (2/199).

[2] Imepokelewa na Al-Ajurri katika kitabu Ash-Sharia (5/2374), 1853.

﴿وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدۡعُونِيٓ أَسۡتَجِبۡ لَكُمۡۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسۡتَكۡبِرُونَ عَنۡ عِبَادَتِي سَيَدۡخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ٦٠﴾

Na Mola wenu Mlezi anasema: Niombeni nitakuitikieni. Kwa hakika wale ambao wanajivuna na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike. [Surat ghaafir 60], Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

﴿إِنَّ ٱلَّذِينَ تَدۡعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ عِبَادٌ أَمۡثَالُكُمۡۖ فَٱدۡعُوهُمۡ فَلۡيَسۡتَجِيبُواْ لَكُمۡ إِن كُنتُمۡ صَٰدِقِينَ ١٩٤﴾

Hakika hao mnao waomba asiye kuwa Mwenyezi Mungu ni waja mfano wenu nyinyi. Hebu waombeni, nao wakuitikieni, kama mnasema kweli. [Al-A'araf: 194], Na amesema Mtukufu:

﴿وَأَنَّ ٱلۡمَسَٰجِدَ لِلَّهِ فَلَا تَدۡعُواْ مَعَ ٱللَّهِ أَحَدٗا ١٨﴾

Na hakika misikiti ni ya Mwenyezi Mungu, basi msimuabudu yeyote pamoja na Mwenyezi Mungu. [Al-Jinn: 18].

Haifai kumuomba Mwenyezi Mungu akiwa kwenye kaburi, na akitaka kuomba asonge mbele na kuliacha kaburi, aelekee Qibla na aombe, na wala haifai kulielekea kaburi anapoomba.

Na amesema Imam Malik, Mwenyezi Mungu amrehemu: "Sioni kusimama mbele ya kaburi la

Mtume - rehema na Amani zimfikie - na kuomba dua."

Haifai kisheria kwenda mara kwa mara kwenye kaburi wakati wa kuingia Msikitini au kutoka humo, si kwa wakaazi wa Madina wala kwa wageni wanaotoka nje yake, kwani kunahofiwa kuwa jambo hilo ni miongoni mwa kulifanya kaburi kuwa Idi.

Na aliyakataza Mtume Rehema na Amani ziwe juu yake hayo, akasema: "Msilifanye kaburi langu kuwa sikukuu, wala msizifanye nyumba zenu kuwa makaburi, na popote mlipo nitakieni rehema, kwani dua zenu hunifikia."[1]

Na maana ya: "Msilifanye kaburi langu kuwa sikukuu" ni kulizuru mara kwa mara katika wakati au hali maalum, kama vile kuihusisha ziara yake kila siku, au wiki, au mwezi, au katika hali maalum inayofanywa kuwa sababu ya kulizuru. Na imesemwa: Yaani, msilifanye kuwa ni msimu mnaokusanyikia[2].

Na amesema Imam Malik, Mwenyezi Mungu amrehemu: "Na haimlazimu mtu wa Madina anayeingia na kutoka Msikitini kusimama kwenye

[1] Ameipokea Ahmad katika Al-Musnad kwa nambari: (8804), kwa isnaad hasan.

[2] Tazama: "Al-Mufradaat", cha Ar-Raaghib Al-Asfahaaniy (ukurasa wa 594), na "Sharh as-Suduur bi Tahriim Raf' al-Qubuur", cha Ash-Shawkaaniy (ukurasa wa 16).

kaburi, bali hilo ni kwa wageni."[1]

Na kauli yake Mwenyezi Mungu amrehemu: "Na hakika hilo ni kwa wageni": Yaani, ziara kwa ujumla, sio kurudiarudia ziara wakati wa kuingia na kutoka.

Asisimame mbele ya kaburi kama anavyofanya mtu anayeswali kwa kuweka mkono mmoja juu ya mwingine kifuani au chini yake; kwa kuwa namna hii ni maalum kwa ajili ya Swala, nayo ni namna ya kujidhalilisha na kunyenyekea isiyofaa isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mtu asilielekee kaburi kwa mbali ili kumtolea salamu Mtume, rehema na amani ziwe juu yake, kama wanavyofanya baadhi ya watu; kwa sababu jambo hili hawakuwa wakilifanya Maswahaba, Mwenyezi Mungu awawie radhi, wala watangulizi wema miongoni mwa Maimamu wanne na wengineo.

Haifai kulielekea Kaburi Tukufu kwa dua wala kwa kisomo cha Qur'ani na mfano wa hayo kutoka upande wowote ule; hili ni sawa na yale yaliyotangulia miongoni mwa mambo ya uzushi. Na haifai kwa Muislamu kuzua katika dini yake yale ambayo Mwenyezi Mungu hakumruhusu. Na Imam Malik, Mwenyezi Mungu amrehemu, alikataza mambo

[1] Al-shifaa li Al-qaadhiy 'Iyaadh (juzuu 2/204), Al-madkhal li Ibni Al-hajj (juzuu 1/262).

yanayofanana na kitendo hiki, na akasema: “Watu wa mwisho wa Umma huu hawatatengemaa isipokuwa kwa yale waliyotengemaa kwayo wa mwanzo wake.”[1]

Kutojishughulisha na kupiga picha na kurusha matangazo ya moja kwa moja wakati wa kumsalimu Mtume ﷺ.

Na rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Mtume wetu Muhammad na ali zake na Maswahaba zake.

❋❋❋

[1] Tazama: Mkusanyo wa Fatwa za bin Baaz, 16/110.

Yaliyomo

Fadhila na adabu za Msikiti wa bwana Mtume na hukumu za kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na kaburi za Maswahaba zake wawili, Mwenyezi Mungu awe radhi nao 2

Utangulizi 2

Ya kwanza: Fadhila za Msikiti wa Mtume 3

Pili: Inapendekezwa kuutembelea Msikiti mtukufu wa Mtume 6

Tatu: adabu za kuutembelea Msikiti wa Mtume 6

Ya nne: Hukumu na adabu za kuzuru kaburi la Mtume, rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na makaburi mawili ya Maswahaba zake wawili, Mwenyezi Mungu awe radhi nao. 15

❋❋❋

sw492v1.0 - 02/11/2026

رئاسة الشؤون الدينية بالمسجد الحرام والمسجد النبوي

رسالة الحرمين

Ujumbe wa Haramain

Yaliyomo ya Muongozo wa Kishari'ah kwa
Wanaokusudia Msikiti wa Makkah na
Msikiti wa Mtume kwa Lugha Mbalimbali